## K ITALU CHA TUMBAKU



**Kwa maelezo zaidi wasiliana na TORITA:**

**S.L.P. 431, Tabora , Simu/Fax**

+255 732 988 245

**Barua pepe: info@torita.or.tz**

**Tovuti: www.torita.or.tz**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO
CHAKULA NA USHIRIKA

**TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU TANZANIA (TORITA)**

# CONFIDOR 70WP



# CONFIDOR 70WP

## 1.0 Utangulizi

Tumbaku nizao ambalo huathiriwa na wadudu waaribifu. Wadudu ambao hupatikana katika udongo,mbegu ya tumbaku,shina, majani na maua . Mkulima hupata hasara kubwa kwani kilo nyingi za tumbaku hupotea kutokana na uharibifu huo wa wadudu.
Kwakuwa ubora wa tumbaku huanzia katika kitalu cha tumbaku hivo ni muhimu sana kuzingatia kanuni za utunzaji wa kitalu ilikupata tumbaku nyingi na yenye ubora

CONFIDOR (30GM PACKET) ni kiuadudu cha kudhibiti wadudu mbalimbali waharibifu wa tumbaku hususani chawa na mchwa wa haribifu wa tumbaku.

**2.0 Viwango vya viuatilifu:**

Imidachloprid 70 WP

**3.0 Wadudu wanaodhibitiwa:**

Hasa dawa hii huthibiti chawa na mchwa wa tumbaku katika kitalu cha tumbaku

**4.0 Jinsi ya kutumia**

i. Pima kiasi cha lita 20 za maji katika chombo safi mfano wa chombo kizuri cha kutumia ni watering can kisha weka 10gm za confidor katika maji na changanya vizuri kabla ya kutumia

ii.Tumia mchanganyiko huu siku ya kusia tumbaku kitaluni

iii. Mchanganyiko wa dawa hii na maji tajwa hapo juu utumike katika bedi la tumbaku lenye urefu wa mita 20M na upana wa mita 1.5M

**5.0. Muda wa kuweka:**

Wakati wa jioni au asubuhi mara tu baada ya kusia tumbaku.

**Angalizo:**

1. Tumia maji safi.
2. Tumia vifaa vya kukinga mwili wakati wa kutumia.Mfano gloves, mask,ovaloli, na rain boot
3. Dawa itunzwe stoo kwenye hali ya ubaridi na ukavu pia weka mbali na watoto
4. Dawa itumike wakati wa asubuhi au jioni ili kuepuka athari zinazoweza kusababishwa na jua kama vile kupotea kwa dawa kwa njia ya mvuke (Evaporation)